

Kuepuka Ulaghai

Ulaghai ni jaribio la uongo la kumhadaa mtu kwa njia ambayo inamnufaisha kifedha mtu anayehadaa, kwa hasara ya mtu anayehadaiwa. Ni muhimu kuelewa aina chache maarufu za ulaghai na kujua jinsi ya kuzitambua.

Ulaghai Maarufu

Hapa chini pana mifano minne ya ulaghai maarufu. Kuna mamia zaidi. Kwa jumla, tahadhari kuhusu simu, barua pepe, au ujumbe wa maandishi unaotoa ofa ambazo ni za kutilia shaka, zinatoa vitisho au shtuma, zimejaa makosa ya hijai na sarufi, au kuomba Taarifa Zinazotambulisha Binafsi (PII).

Fedha za Ushindi Zisizotarajiwa

Katika ulaghai huu, mtu anayehadaiwa anatumwa mawasiliano na kuambiwa kuwa ameshinda pesa, bidhaa, au huduma katika shindano ambalo hakushiriki. Anaombwa atume pesa au PII ili kudai fedha za ushindi. Fedha hizi za ushindi huwa hazitumwi. Ukiwa na PII yako, mtu anayehadaa anaweza kufikia akaunti yako ya benki na kuhamisha akiba yako hadi kwenye akaunti yake binafsi.

Mashirika ya Hisani ya Uongo

Katika ulaghai huu, mtu anayehadaiwa anatumwa mawasiliano na mtu anayejifanya kuwa mwakilishi wa shirika la hisani, ambaye baadaye anaomba pesa. Tafuta mashirika ya hisani mtandaoni ili uthibitishe uhalali wayo na utumie tu vituo salama vya mchango kutoa mchango wa pesa.

Kodi Unazodaiwa

Katika ulaghai huu, mtu anayehadaiwa anapigiwa simu na mtu anayedai kuwa mwakilishi wa Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service, IRS) au tawi jingine la serikali, akitisha kukamatwa au kufukuzwa nchini isipokuwa alipe ada fulani. IRS haitawahi kuomba PII, hivyo usitoe zako! Ukipigiwa simu ya aina hii, angalia nambari ya simu ya anayepiga katika kivinjari chako. Hii itokusaidia kujua ikiwa nambari iliripotiwa awali kuwa ya ulaghai. Ikiwa una wasiwasi, ripoti tukio kwa Msimamizi wako wa Huduma.

Ofa za Kazi Bila Kuziona

Katika ulaghai huu, mtu anayehadaiwa anatumwa mawasiliano na kampuni bandia inayompa kazi kabla hajahojiwa ana kwa ana wala kutuma ombi rasmi. Usiwha kumpa mwajiri mtarajiwa PII yako bila kuthibitisha uhalali wao.

Je, Taarifa ya Kutambulisha Binafsi ni Nini?

Taarifa ya Kutambulisha Binafsi (PII) ni taarifa yoyote ambayo inayoweza kukutambulisha binafsi. Inajumuisha, lakini si tu yafuatayo:

- Nambari za Ruzuku ya Serikali
- Majina Kamili
- Tarehe za Kuzaliwa
- Anwani
- Nambari za Akaunti ya Benki

Je, ni dalili gani zinazoonyesha kuwa ujumbe huu ni wa ulaghai?

Hujambo Bi. Sanchez,

Ujumbe huu unatoka Cleveland Police. Unadaiwa \$2000 za kodi za jiji. Usipolipa pesa hizi kufikia mwisho wa mwezi, UTAKAMATWA!

Afisa ametumwa nyumbani kwako. Anapowasili MUDA UTAKUWA UMEISHA!

Kwa sababu malipo yamechelewa, utahitaji kulipa kwa njia ya kadi ya malipo ya kulipa mapema.



- Sauti isiyo rasmi
- Ombi la kadi ya kulipia mapema

Je, nini kingine?

Kuwafuatilia Watoto

Kama mzazi katika kipindi cha dijitali, kufuatilia shughuli za mtoto wako mtandaoni kunaweza kuwa kugumu. Ni muhimu kuwafunza watoto kuhusu intaneti, ambayo itakuwa sehemu ya maisha yao ya jamii, elimu na taaluma. Wakati uo huo, **ni muhimu kulinda watoto dhidi ya vipengee vyenye madhara kuhusu intaneti, ikijumuisha unyanyasaji mtandaoni, maudhui yasiyofaa, unyanyasaji kifedha na wawindaji watoto mtandaoni.** Udhibiti wa mzazi na zana za kufuatilia ni muhimu kwa kuwalinda watoto wenu.

Misamiati Muhimu

Programu mpya ya Android na iOS (Apple) inajumuisha udhibiti wa mzazi uliojengewa ndani. Programu za ziada za udhibiti wa mzazi zinapatikana bila malipo, au nunua kwenye mifumo ya kusakinisha programu (*kwa maelezo zaidi kuhusu app stores, kagua 1.1*).

Unyanyasaji mtandaoni

Unyanyasaji mtandaoni ni kutuma, kuchapisha, au kushiriki maudhui hasi, yanayodhuru au ya uongo kumhusu mtu kwenye ujumbe wa maandishi, programu, mitando ya jamii, mijadala, au michezo ya video ambapo watu wanaweza kutazama, au kushiriki maudhui na wengine.

Wawindaji Watoto Mtandaoni

Wawindaji watoto mtandaoni ni watumiaji wa mtandaoni ambao ni watu wazima wanaowatumia vibaya watoto kwa kutumia teknolojia ya dijitali kutafuta na kuwalenga watoto.

Vichujio vya maudhui

Zana hizi huzuia watoto kufikia maudhui yasiyofaa kwa umri. Vichujio vya maudhui vinapatikana kwenye programu, vifaa na vivinjari vingi.

Vidhibiti vya Matumizi

Vidhibiti hivi huzuia muda ambao watoto wanafikia programu fulani, saa ambazo wanatumia programu fulani na ikiwa wanaweza au hawawezi kufikia programu kabisa.

Zana za Ufuatiliaji

Zana hizi huwaruhusu wazazi kufuatilia eneo la vifaa, kuona kile ambacho watoto wanafanya vifaa vyao na kujifunza kuhusu vipengee vingine vya matumizi yao.


Kitu cha Kuangazia

Kuna njia nyingi ambazo watoto na vijana wanaweza kutumia kwenye intaneti. Kama wazazi, kuelewa unyanyasaji mtandaoni na wawindaji watoto mtandaoni kunaweza kukusaidia kuzuia.

Programu na michezo mingi huonekana kwenye ununuzi ndani ya programu. Hizi huwaruhusu watoto kufanya ununuzi halisi wa fedha. Inapowezekana, zua ununuzi wa ndani ya programu kwa kusasisha mipangilio ya udhibiti wa mzazi na kuepuka kuunganisha taarifa yako ya benki kwenye duka la programu.

Maudhui ya vurugu, ngono, au yasiyofaa yanapatikana kila mahali kwenye intaneti. Mwepushie mtoto wako hatari kwa kukagua tovuti, michezo na programu kabla ya kuwaruhusu watoto wako kuzitumia.

Inawezekana kumwepushia mtoto wako hatari ya maudhui yanayodhuru, lakini si kuyazuia kikamilifu. **Hakikisha kuwa umejadili usalama wa intaneti na watoto wako moja kwa moja.** Stadi hizi nyingi zitakuwa muhimu katika vipengee vingine vya maisha yao.



Kudhibiti Historia yako ya Dijitali

Historia yako ya dijitali ni rekodi ya elektroniki ya kila kitu unachokifanya kwenye intaneti. **Kila ujumbe wa maandishi, barua pepe, machapisho ya mitandao ya jamii, picha, ununuzi na mambo unayotafuta kwenye intaneti huhifadhiwa milele.** Kuna safu mbili za historia hii ya dijitali. Safu ya kwanza ni taarifa zinazoweza kufikiwa na mtumiaji yeyote wa intaneti. Ya pili, ni taarifa zinazoweza kufikiwa na Mtoaji Huduma wako wa Intaneti, mashirika, serikali na wahalifu wa mtandaoni. Ni muhimu kuelewa jinsi taarifa hizi zinavyokusanya, zinachowea kufanyiwa na jinsi ya kuzidhibiti.

Misamiati Muhimu

Matangazo Maalum

Tovuti nyngi hutumia historia yako ya jumla ya dijitali kutangaza bidhaa kutoka kwenye tovuti ulizotembelea awali.

Mtandao wa Faragha wa Dijitali (Virtual Private Network, VPN)


VPN hukupa faragha mtandaoni kwa kuuunda mtandao wa faragha kutoka kwenye muunganisho wa intaneti ya umma. VPN husaidia kuzuia wahalifu wa mtandaoni kuingilia data unayotuma na kupokea kutoka kwenye kifaa chako. Visambaza data vingi vya intaneti vina VPN. Kuweka VPN kunaweza kugharimu ada kidogo ya kila mwezi (*kwa maelezo zaidi kuhusu visambaza data, pitia 1.2*).

Kuvnjari kwa Faragha (Hali ya Chinichini)

Unapotumia kivnjari cha intaneti, kinaweza kurekodi unachofanya, kuhifadhi manenosiri na taarifa za fedha na kupakua vidakuzi kutoka kwenye tovuti ulizotembelea awali. Kuvnjari kwa faragha huzuia baadhi ya mambo haya na ni muhimu haswa kutumia ukiwa kwenye kompyuta inayotumiwa na watu wengi.

Vidakuzi

Vidakuzi ni data iliyotumwa kutoka kwenye kivnjari cha intaneti na kuhifadhiwa kwenye kompyuta yako. Hatua hii huruhusu tovuti kukumbuka na kurekodi manenosiri na historia ya kuvnjari. Tovuti ikikuonya kuwa hutumia vidakuzi, kwa kutumia tovuti unaipa ruhusa kufikia historia yako ya jumla ya dijitali, hatua inayoweza kusababisha kutumiwa matangazo yanayokulenga.



Historia Yako Msingi ya Dijitali

Waajiri na wenyewe nyumba wanaweza kutafuta kwenye akaunti ya mitandao ya jamii ya mwajiriwa au mpangaji mtarajiwa ili kupata maelezo zaidi kumhusu.

Mwajiri akipata akaunti yako ya Twitter, Facebook au Instagram, atafikiria nini?

Ili kudhibiti historia yako msingi ya dijitali, unaweza kufanya mambo mawili. Kwanza, weka mipangilio yako ya faragha unayopendelea kwenye akaunti zako zote za mitandao ya jamii. Pili, **chapisha tu kitu ikiwa huna tatizo kila mtu akikiona**. Kuna uwezekano wa wao kukiona wakati wowote!

Historia Yako ya Jumla ya Dijitali

Si tu kile unachokusudia kuweka hadharani kinachobadilisha historia yako ya dijitali. Mashirika, mamlaka ya kutekeleza sheria, serikali na wahalifu wa mtandaoni hukusanya taarifa kutoka kwa watumiaji wa intaneti. **Taarifa zako zinaweza kutumiwa kwa njia nyngi, kuanzia kuunda matangazo yanayokulenga hadi kuiba kitambulisho chako.**

Ni wakati gani ambapo shirika linaweza kutoa taarifa zilizo kwenye historia yako ya dijitali kwa mamlaka ya kutekeleza sheria? Je, ni halali?

Ingawa ni halali kwa mashirika kushiriki historia yako ya dijitali, baadhi ya kampuni zina sera zinazopinga hatua hiyo. Unaweza kulinda historia yako ya dijitali kwa kutumia huduma ya VPN kuficha uwepo wako mtandaoni, kuvnjari katika hali ya faragha ili kuzuia vidakuzi na kuwa mwangalifu kwa kile unachokifanya mtandaoni!

Programu Hasidi, Virusi, Ulinzi dhidi ya Virusi na Kinga Mtandao

Kuna njia nyingi ambazo walaghai na wahalifu wa mtandaoni wanaweza kutumia kufikia taarifa zako. Pindi wanapofikia kifaa chako, au kufuatilia Taarifa Zinazokutambulisha Binafsi, wanaweza kufungua akaunti za mkopo kwa jina lako, kutoza ununuzi kwenye akaunti yako ya hundi na kuiba pesa kwenye akaunti yako ya akiba. Virusi na programu hasidi ni zana msingi zinazotumiwa kuwasaidia wahalifu katika jitihada hizi. **Kilinde kifaa chako na ujilinde kwa programu za kuzuia virusi na kinga mtandao!**

Misamiati Muhimu

Programu Hasidi

Programu hasidi ni aina yoyote ya programu mbaya iliyoundwa ili kupata idhini ya kufikia, au kuharibu kifaa cha elektroniki. Mara nyingi huwa imeundwa ili kuiba pesa. Virusi vya kompyuta ni aina ya programu hasidi inayoruhusu wahalifu wa mtandaoni kufikia taarifa zako za benki na kuvuruga muamana wako (*kwa maelezo zaidi kuhusu muamana, pitia 4.1*).

Virusi vya Kompyuta

Virusi vya kompyuta ni programu hasidi, au msimbo, unaokusudia kubadilisha jinsi kifaa kinavyofanya kazi. Virusi vinaweza kusambaa baina ya vifaa vilivyounganishwa, kuiba manenosiri, kurekodi mibonyezo ya kibodi, faili mbou, wawasiliani wa barua pepe taka na hata kumiliki kifaa. Husambaa kuitia viambatisho vya barua pepe, faili na programu zilizopakuliwa na maudhui ya mitandao ya jamii yaliyoshirikiwa.

Ulinzi dhidi ya Virusi

Kampuni mbalimbali, kama vile Norton, huunda programu za kuzuia virusi. Vifurushi hivi vya programu zinazoweza kupakuliwa hugharimu ada ya kila mwezi, lakini hutoa ulinzi thabiti dhidi ya programu hasidi na virusi.

Kinga Mtandao

Kinga mtandao ni sawa na programu ya kuzuia virusi kwa muunganisho wako wa intaneti. Hufuatilia na kudhibiti trafiki ya mtandao inayoingia na kutoka. Pia huweka vizuizi baina ya mitandao ya ndani ya kuaminika na mitandao ya nje isiyoaminika.



Ishara za Kuonyesha Kuwa Huenda Una Virusi

- Madirisha ya kuibuka mara kwa mara
- Mabadiliko kwenye ukurasa wako wa mwanzo
- Barua pepe zilizotumwa kutoka kwenye akaunti yako ambazo hukuandika
- Kompyuta au programu kuacha kufanya kazi mara kwa mara
- Utendakazi uliopungua kuliko kawaida
- Programu zisizojulikana kwenye kifaa chako
- Shughuli zisizo za kawaida



Jinsi ya Kuzuia Virusi na Programu Hasidi

- Usibofye kwenye matangazo yanayoibuka
- Tumia miunganisho salama ya mtandao na usishiriki skrini wala kuunganisha kompyuta ambazo hazina ulinzi dhidi virusi.
- Kagua faili kila wakati kabla ya kuzipakua
- Tumia programu unayoamini ya ulinzi dhidi ya virusi

Taarifa za Kupotosha

Intaneti imerahisisha kupatikana kwa taarifa. Huruhusu pia usambazaji wa taarifa kwa haraka. Leo, unaweza kupata taarifa kwa urahisi kuhusu matukio ya sasa mtandaoni, lakini **si kila kitu unachosoma kwenye intaneti ni cha kweli**. Iwe umepata taarifa yako kwenye mitandao ya jamii au chanzo cha habari, unapaswa kuangalia usahihi wa unachosoma mtandaoni ili kuthibitisha ikiwa ni za kweli.

Habari Bandia

Habari bandia ni kauli ya kisasa inayoeleza taarifa za kupotosha kwenye mitandao ya jamii, kama vile Facebook na Twitter. Kauli sasa inatumiwa sana na watu na vyombo vya habari, Habari bandia inamaanisha kuwa taarifa ni za uongo na hazina vyanzo, wala manukuu ya kuweza kuthibitisha. Habari bandia zinaweza kumaanisha kosa. Kwa mfano, ikiwa chanzo cha habari kinashiriki taarifa ambazo hazikuangaliwa usahihi, ambazo kitatambua baadaye kuwa za uongo. Habari bandia zinaweza pia kuwa taarifa za uongo zinazoshirikiwa makusudi. Watu wanaweza hata kukiita kitu kuwa habari za uongo ilhali ni cha kweli.

Kwa wale wasiofahamu intaneti, vyanzo vingi vya vyombo vya habari vya tashtiti au kijembe huonekana kuwa kweli. Taarifa kwenye mifumo ya tashtiti si halisi. Mfumo unaojulikana sana wa tashtiti ni Onion – unaweza kusoma kwenye theonion.com.

Taarifa za kupotosha si rahisi kutambua kila wakati. **Tumia vyombo vya habari vya kuaminika na visivyoegemea upande wowote kuwa chanzo chako cha habari.** Unaweza kuchagua kutembelea moja ya programu za wavuti zifuatazo zinazoaminika kwa ajili ya habari zako: New York Times, Wall Street Journal, Washington Post, National Public Radio (NPR), Economist, New Yorker, Reuters, Atlantic, au Politico.

Hatimaye, chanzo cha chombo cha habari unachopendelea ni uamuzi wako. Jaribu kusoma mitazamo tofauti. Kwa mfano, labda chombo cha habari unachopendelea kiliorodheshwa hapo juu. Ikiwa ndivyo, zingatia kusoma chanzo cha habari cha kimataifa pia kama vile BBC. Hatua hii itatoa mtazamo wa Marekani na wa kimataifa kuhusu habari na kukuruhusu kuwa na maoni yako kuhusu siasa, serikali na matukio mengine ya kisasa.

Kutambua Taarifa za Kupotosha

Hakuna njia rahisi ya kutambua taarifa za kupotosha, lakini unaweza kuanza kwa kuchukua hatua zifuatazo:



- Jiulize maswali kuhusu unachokisoma
- Elewa mifumo ambayo hutoa taarifa za kupotosha mara kwa mara
- Chunguza ukweli

Unaweza pia kutumia programu, kama vile kuangalia usahihi kupitia Reuters ili kutambua taarifa za kupotosha:
www.reuters.com/fact-check.

Taarifa kupita kiasi

Machi 2020, Shirika la Afya Duniani (Word Health Organization, WHO) lilitaja taarifa za kupotosha kwenye intaneti kuhusu janga la virusi vya korona kuwa ‘taarifa kupita kiasi.’ Ili kukabiliana na taarifa za kupotosha zinazopatikana kwenye mitandao ya jamii, WHO ilianza kampeni ya kudhihirisha uvumi ulioenea kote kuhusu virusi vya korona. Kwa mfano, kula kitunguu saumu kulinda watu dhidi ya kupata virusi vya korona.

